



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA



(57)

HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)

Simu Na 2988305/2988324

Nukushi Na. 2988258

Barua pepe: ded@urambodc.go.tz

Tovuti: www.urambodc.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na.UDC/W.I/254/VOL.I/57

Mkurugenzi Mtendaji (W)

S.L.P 170,

URAMBO.

TABORA.

Tarehe: 31/08/2020

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Urambo kwa kushirikiana na taasisi ya Management and Development for Health (MDH) anawatangazia watu wote wenye sifa kuomba nafasi za kazi za mkataba. Nafasi hizi za ajira ya mkataba zinafadhiliwa na taasisi ya Management and Development for Health (MDH) ambayo imekuwa ikishirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Urambo katika utoaji wa huduma za afya hasa katika harakati za utoaji wa huduma za kupambana dhidi ya maambukizi ya VVU na Ukimwi pamoja na athari zake.

1.0 MSAIDIZI WA TAKWIMU (DATA CLARK) NAFASI SABA (07)

1.1 SIFA ZA MWOMBADI

Mwaombaji anatakiwa awe na Elimu ya kidato cha nne (IV) au sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya) Astashahada (Certificate), Stashahada (Diploma) au Shahada (Bachelor Degree) katika moja ya fani zifuatazo:-

Fani ya takwimu (Statistics), Utunzaji wa Kumbukumbu (Records Management), Utunzaji wa takwimu za kielektroniki za kiafya (Health Records Management) au Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.

1.2 SIFA ZA ZIADA/UZOEFU

Wenye uzoefu zaidi ya mwaka mmoja katika matumizi sahihi ya Takwimu na mifumo ya kutolea taarifa za Afya watapewa kipaumbele.



1.3 KAZI/MAJUKUMU YA KARANI TAKWIMU (DATA CLARK)

- i. Kukusanya takwimu na kuziingiza kwenye mfumo wa kompyuta (**CTC2 Data base**).
- ii. Kutunza takwimu na taarifa zote zilizomo kwenye mfumo wa kompyuta.
- iii. Kutunza, Kupanga na kuhifadhi vizuri majalada ya wateja.
- iv. Kuhakikisha Takwimu zote zilizoingizwa kwenye mfumo na ubora na usahihi.
- v. Awe na uwezo wa kutunza siri za wateja anaowahudumia.
- vi. Awe tayari kufanya kazi na kuishi katika mazingira yoyote hasa vijiji.
- vii. Kutoa taarifa endapo kuna matatizo yatakayotokea kwa msimamizi wa kazi.
- viii. Kufanya majukumu yote anayopangiwa na msimamizi wa kazi.

2.0 MASHARI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE

- xi. Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania na wenye Umri usiozidi miaka 45.
- xii. Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa.
- xiii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu.
- xiv. Maombi yote yaambatanishwe na picha 2 (Passport size) nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa zilizoelekezwa hapo juu.
- xv. "Testimonials", "Provisional Results", "Statement of Result", "hati za matokeo kidato cha nne na sita" (FORM IV AND FORM VI RESULT SLEEP) **HAVITAKUBALIWA**.
- xvi. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamalaka husika (TCU, NACTE na NECTA).
- xvii. Mwisho wa wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **14 Septemba, 2020 saa 9:30 Alasiri**.
- xviii. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA**.
- xix. Maombi yote yatumwe au kuwasilishwa katika masjala bayana ya Mkurugezi Mtendaji Wilaya ya Urambo kwa anwani ifuatayo:-
Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
Halmashauri ya Wilaya ya Urambo,
S.L.P 170,

URAMBO

Absalama A. Kajuna
Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Wilaya
Halmashauri ya Wilaya
Urambo

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILA
URAMBO